# CHAMA CHA USHIRIKA CHA DUNIA YETU

# (DUNIA YETU COOPERATIVE SOCIETY LTD)

# MASHARTI YA CHAMA

**Masharti haya yameandaliwa na Bodi ya**

**Dunia Yetu Cooperative Society Ltd**

**S.L.P 6972**

**DAR ES SALAAM** **Toleo la I - July, 2024**

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

*1. Jina la Masharti*

1. Masharti haya yatajulikana kama "Masharti ya Chama cha DUNIA YETU COOPERATIVE SOCIETY LTD.

*2. Tafsiri ya Maneno*

(1) Katika masharti haya, isipokuwa kama imefafanuliwa vinginevyo katika sharti husika, maneno yafuatayo yatakuwa na maana kama ifuatavyo:

"Kamati anzilishi" maana yake ni Bodi iliyochaguliwa kuongoza Chama kwa mara ya kwanza kabla ya Chama kupata usajili na kabla ya Bodi ya uongozi kuchaguliwa;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya uongozi wa Chama iliyochaguliwa na mwanachama kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika.

"Chama" maana yake ni Chama cha Ushirika cha Dunia Yetu Cooperative Society Ltd ambacho kitakuwa na jukumu na kutoa muongozo kulingana na Sheria na Kanuni za Ushirika.

"Kanuni za Vyama Vya Ushirika" maana yake ni Kanuni za Vyama Vya Ushirika za Mwaka 2015 zilizotolewa katika Gazeti la Serikali kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 272 la Mwaka 2015.

"Sheria ya Vyama Vya Ushirika" maana yake ni Sheria ya Vyama Vya Ushirika Namba 6 ya Mwaka 2013;

(2) Katika Masharti haya maneno yaliyotumika katika umoja yatakuwa na maana ile yakitumika katika wingi na hivyo maneno yaliyotumika katika wingi yatakuwa na maana ile ile yakitumika katika umoja.

(3) Iwapo kutatokea kukinzana baina ya tafsiri ya maneno yaliyoko katika Masharti haya na tafsiri iliyoko katika Sheria ya Vyama Vya Ushirika au Kanuni za Vyama Vya Ushirika, tafsiri iliyoko katika Sheria au Kanuni, kadri itakavyokuwa, ndiyo itakayofuatwa.

3. *Jina, Anuani na Makao Makuu ya Chama*

(1) Jina la Chama litakuwa Dunia Yetu Cooperative Society Ltd.

(2) Anuani ya Chama itakuwa S.L.P 6972 Dar es Salaam.

(3) Ofisi na Makao Makuu ya Chama itakuwa katika Wilaya ya Kinondoni, jengo la Dora Tower, Mwenge, jijini Dar es Salaam.

4. *Fungamano la Pamoja na Eneo la shughuli za Chama*

(1) Fungamano la pamoja litakuwa ni wanateknolojia.

(2) Eneo la shughuli la Chama cha Ushirika cha Dunia Yetu Cooperative Society LTD litakuwa wilaya ya Kinondoni.

## SEHEMU YA PILI

## DIRA, DHIMA NA MADHUMUNI YA CHAMA

5. *Dira na Dhima ya Chama*

(1) Dira ya Chama ni "Kuona vijana wa Tanzania wanakua na kudumisha maisha yao kupitia teknolojia na kuboresha ujuzi na taaluma ili wazidi kujijenga na kuimarika".

(2) Dhima ya Chama ni "kuhamasisha, kuwaunganisha wanataaluma wote wa kiteknolojia na kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika uwekezaji wa shughuli za kiteknolojia"

6. *Lengo na Madhumuni ya Chama*

(1) Lengo kuu la Chama ni kuwaunganisha wanataaluma wote wa kiteknolojia na kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika uwekezaji wa shughuli za kiteknolojia.

(2) Bila kuathiri lengo tajwa hapo juu, madhumuni ya Chama yatakuwa ni pamoja na:-

a.Kuwezesha maendeleo, uzalishaji, au usambazaji wa suluhisho za kiteknolojia za uvumbuzi kwa manufaa ya pamoja ya wanachama wake na jamii inayowazunguka;

b.Kutoa elimu na mafunzo yanayolenga teknolojia kwa wanachama na jamii kuhusu teknolojia inayobadilika na stadi za dijitali kama vile uandishi wa nambari na maendeleo ya programu;

c.Kushiriki katika shughuli zinazohusiana na teknolojia ambazo zinahimiza maendeleo endelevu ndani ya jamii yetu;

d.Kudumisha viwango vya maadili katika uvumbuzi wa kiteknolojia; na

e.Kusaidia juhudi za kiteknolojia ambazo zinaimarisha ubora wa maisha na ustawi wa wanachama wetu na jamii kwa ujumla kupitia suluhisho za uvumbuzi.

f.Kusimamia mgahawa, kuchangisha fedha, kusaidia kuanzisha kwa teknolojia mpya na kurahisisha miradi kupitia ubunifu wa watu mbalimbali.

## SEHEMU YA TATU

## UANACHAMA

7. *Uanachama na sifa ya kuwa mwanachama*

(1) Uanachama katika Ushirika huu utakuwa wazi kwa wanataaluma wote wa kiteknolojia.

(2) Bila kuathiri matakwa ya Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika, yeyote anayekusudia kuwa Mwanachama wa Ushirika huu ni sharti:-

a.Awe na umri wa miaka 18 au Zaidi

b.Awe raia wa Tanzania

c.Awe na uwezo wa kulipa kiingilio na michango kwa mujibu wa Masharti haya;

d.Awe tayari kushirikiana na mwanachama wengine katika Ushirika huu katika kufanikisha lengo na madhumuni ya Chama;

e.Awe tayari kusimamia na kutekeleza matakwa ya Sheria ya Vyama Vya Ushirika, Kanuni na Masharti ya Vyama Vya Ushirika,

f.Wanachama walioshiriki katika shughuli za awali wakati wa kuandikishwa kwa Ushirika huu, ambapo majina yao yameorodheshwa katika Jedwali la Kwanza la Masharti haya, vitatambulika kama "Mwanachama Anzilishi".

8. *Utaratibu wa kujiunga na Chama*

Mwanataaluma yeyote anayekusudia kujiunga na Chama/Ushirika huu anapaswa kufanya yafuatayo:

a.Awe tayari kushiriki mafunzo ya elimu za Ushirika.

b.Atajaza fomu ya maombi ya kujiunga na Chama.

c.Maombi ya uanachama yatapaswa kujadiliwa na Bodi ya Chama ambayo itatoa pendekezo kwa Mkutano Mkuu ambao utakuwa na uamuzi wa mwisho juu ya maombi hayo.

9. *Haki za Mwanachama*

Bila kuathiri matakwa ya Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika, mwanachama atakuwa na haki zifuatazo: -

a.Kuchagua na kuchaguliwa kuwa kiongozi wa Chama;

b.Kuhudhuria na kushiriki katika Mikutano ya Chama;

c.Kuitisha Mkutano Mkuu Maalum wa Chama kwa kufuata taratibu zilizoainishwa katika Kanuni za Vyama Vya Ushirika pamoja na Masharti haya;

d.Kupatiwa huduma stahiki za Chama baada ya kukidhi vigezo vinavyotakiwa;

e.Kushiriki katika kufanya maamuzi ya Chama;

f.Kupatiwa taarifa zinazokihusu Chama;

g.Kushiriki katika kufanya marekebisho ya Masharti ya Chama;

h.Kujitoa katika Chama; na

i.Haki nyingine zozote zitakazotolewa kwa wengine kwa kuzingatia vigezo na Masharti yaliyokubaliwa.

10. *Wajibu wa Mwanachama*

Bila kuathiri matakwa ya Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika, mwanachama atakuwa na wajibu wa:-

a.Kutoa michango yote iliyokubalika kwa wakati;

b.Kuhudhuria vikao vyote vilivyoidhinishwa na kutoa maoni, mapendekezo, kukosoa na kukubali kukosolewa katika vikao vya Chama;

c.Kutafuta fursa za kiteknolojia, kushiriki katika shughuli za kuchangisha fedha, kushiriki katika miradi ya inkubesheni (incubation), na kuhudhuria warsha zinazolenga suluhisho za teknolojia ya kifedha;

d.Kutoa msaada kwa wanachama kulingana na taratibu zilizokubalika; na

e.Kuheshimu maamuzi ya vikao na taratibu za Chama.

11. *Kukoma kwa uanachama*

(1) Bila kuathiri matakwa ya Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika, mwanachama atakoma kuwa mwanachama kwa:

a.Kujiondoa kwa hiari baada ya kutoa notisi ya siku 60 na kulipa madeni anayodaiwa ama kudhamini;

b.Kupoteza sifa kwa kutojihusisha na shughuli za Chama kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Masharti ya Chama hiki, na kufukuzwa uanachama kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika na Masharti ya Chama.

(2) Mwanachama yeyote hataweza kufukuzwa uanachama isipokuwa baada kupewa notisi ya siku thelathini (30) ikieleza sababu na kusudio la kumwachisha uachama ili kupata haki ya kujibu, kusikilizwa na kujitetea kabla ya kujadiliwa katika Mkutano Mkuu kwa maamuzi ya mwisho. Pia atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika.

(3) Mwanachama anayekoma uanachama anaweza kurejeshewa uanachama wake iwapo ataomba kwa maandishi na kurekebisha dosari zilizosababisha uanachama wake kukoma na iwapo Mkutano Mkuu wa Chama utaridhia.

## SEHEMU YA NNE

## MAPATO NA MATUMIZI YA CHAMA

12. *Mapato na Mali za Chama*

(1) Bila kuathiri matakwa ya Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika, Chama kitakuwa na Vyanzo mbalimbali Vya mapato ikiwa ni pamoja na:-

a.Viingilio Vya mwanachama;

b.Ada ya mwaka;

c.Mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa mbalimbali za kiteknolojia;

d.Michango ya wadau mbalimbali na Mapato mengineyo yatakayopatikana kutokana na shughuli na Vyanzo mbalimbali;

e.Mapato kutokana na uwekezaji wa muda mfupi kwenye uwekeza wenye lengo la kuiva; na

f.Gawio kutokana na kununua hisa kwenye taasisi nyingine.

(2) Chama kitakuwa na Daftari la Mali za Chama ambamo kutaorodheshwa mali zote za Chama ikiwa ni pamoja na:

a.Fedha taslimu;

b.Fedha zilizoko Benki au katika taasisi nyingine za fedha;

c.Magari, Vifaa na zana mbalimbali; na

d.Mali nyingine za Chama.

13. *Ada ya Uanachama na Michango ya Kila Mwezi*

(1) Ada ya Uanachama: Ada ya kiingilio cha chini kabisa ni shilingi laki mbili na nusu (250,000/= TZS), lakini mtu ana uhuru wa kutoa kiasi kikubwa zaidi.

(2) Kiwango cha chini cha michango ya kila mwezi ni shilingi elfu ishirini (20,000/= TZS), lakini mtu ana uhuru wa kutoa kiasi kikubwa zaidi.

(3) Kiasi cha michango kitafanyiwa uamuzi kila mwaka katika kikao cha kwanza cha mwaka husika.

(4) Kukiuka Masharti ya Michango:

-Mwanachama ambaye hatalipa michango yake kwa miezi sita mfululizo bila sababu halali (kama vile kazi, ugonjwa, safari, au msiba) atapigwa marufuku kwa miezi sita na hatakuwa na haki ya kupata stahiki yoyote wakati huo. Akilipa deni ndani ya kipindi cha adhabu ya miezi sita, anaweza kurudishiwa uanachama.

-Mwanachama aliyesimamishwa lazima aombe uanachama upya ikiwa deni litadumu zaidi ya miezi sita bila kulipwa, na kutofanya hivyo kutapelekea kufukuzwa moja kwa moja.

-Mwanachama aliyeondolewa au kurudishwa atakuwa na jukumu la kulipa ada ya kipindi cha uanachama wake tu. Hakuna ada inayotakiwa wakati wa kusimamishwa.

14. *Matumizi ya fedha na Mali za Chama*

(1) Chama kitatumia fedha zake kwa kuzingatia Makisio ya Mapato na Matumizi yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu na kuidhinishwa na Mrajis wa Vyama Vya Ushirika Kwa kuzingatia matakwa ya Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika.

(2) Bila kuathiri matakwa ya sharti hili, Matumizi ya Chama yatapaswa kuzingatia Kanuni za Fedha za Chama na hayatatakiwa kukiuka kasma na kiwango kilichoruhusiwa na Ofisi ya Mrajis wa Vyama Vya Ushirika.

15. *Miradi ya Pamoja au Ushirikiano wa Kiteknolojia*

Chama kinaweza kuingia katika miradi ya pamoja (Joint Ventures) au ushirikiano wa kiteknolojia na taasisi nyingine, chini ya idhini ya Uongozi na kutekeleza makubaliano rasmi yanayobainisha majukumu, dhamana, na faida husika.

16. *Sera za Malipo ya Per Diem*

Malipo ya per diem kwa safari za kikazi na matumizi mengine ya kikazi yatazingatia viwango vilivyoidhinishwa. Malipo hayo yatahitaji kuwasilishwa kwa risiti au nyaraka halali kwa Kamati ya Fedha na Bajeti kwa ajili ya fidia.

17. *Uwekezaji na shughuli za biashara*

(1) Bila kuathiri matakwa ya Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika na Masharti haya, Chama kinaweza kuwekeza au kufanya shughuli za kibiashara zinazohusiana na shughuli za mwanachama wake ili kufanikisha lengo na madhumuni ya Chama kama yalivyoainishwa katika Masharti haya.

(2) Bila Kuathiri matakwa ya sharti hili, shughuli zote za uwekezaji za Chama, kwa mfano UTT-AMIS au Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), zitasimamiwa na Dunia Yetu Cooperative Society LTD ili kuhakikisha Chama kinafikia malengo ya faida kwa manufaa ya wanachama wote.

18. *Ufadhili na Michango ya Hiari*

(1) Mwanachama yeyote aliye na nia ya kusaidia Chama, kutoa mchango, au michango ya hiari kwa Chama, anakaribishwa kwa ukamilifu na wakati wowote.

(2) Michango ya hiari itapokelewa na Mweka Hazina na kutolewa ripoti kwa Katibu ambaye atakijulisha Chama.

(3) Hakuna masharti au kanuni zinazosimamia michango ya hiari, wala matokeo yanayotokana na michango hii.

19. *Utunzaji wa Fedha*

(1) Fedha za Chama zitahifadhiwa CRDB Bank kutumia akaunti ya Chama ambapo watu wawili (2) watatia saini (Signatories) watakaochaguliwa na Chama, mmoja kati yao ataweka saini ili pesa ziweze kuchukuliwa kutoka kwenye akaunti (Either to sign).

(2) Chama kinaweza kubadilisha benki kulingana na fursa zinazotolewa na benki zingine.

## SEHEMU YA TANO

## UONGOZI NA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA CHAMA

20. *Utawala*

Muundo wa Uongozi ni kama ifuatavyo:

a) Mwenyekiti

b) Makamu Mwenyekiti

c) Katibu

d) Katibu Msaidizi

e) Mweka Hazina

21. *Majukumu ya Uongozi*

a) Mwenyekiti

-Kuongoza vikao vyote vya Dunia Yetu

-Kuwa mmojawapo wa watia saini katika akaunti ya Dunia Yetu

-Kuwa mwakilishi wa Chama kwenye shughuli zinazohitaji uwakilishi

-Kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya Dunia Yetu

-Kutekeleza majukumu mengine kwa busara yake na kwa idhini ya wanachama

b) Makamu Mwenyekiti

-Kusimama badala ya Mwenyekiti na kutimiza majukumu yote ya Mwenyekiti wakati Mwenyekiti hayupo

-Kumshauri Mwenyekiti katika kufanya maamuzi magumu katika vikao

-Kuhakikisha mawasiliano ya mara kwa mara na Mwenyekiti ili kuhakikisha ufahamu kamili wa mambo yanayoendelea katika Dunia Yetu

c) Katibu

-Kuwa mtendaji mkuu wa Dunia Yetu

-Kutunza kumbukumbu zote za Chama

-Kuandika na kutunza "minutes" za vikao vyote

-Kuandaa ajenda za vikao kwa ushauri wa wanachama

-Kupokea na kutoa taarifa zote za bajeti na mwenendo wa Chama kutoka Kamati ya Fedha na Usimamizi wa Bajeti

d) Katibu Msaidizi

-Kukaimu nafasi ya Katibu pale ambapo Katibu hayupo

-Kumsaidia Katibu katika kuhakikisha majukumu yote ya ukatibu yanatekelezwa kikamilifu

e) Mweka Hazina

-Kuwa msimamizi wa fedha na mali zote za Dunia Yetu na kuhifadhi rekodi zake

-Kupokea na kulipa fedha za Chama kama ilivyo idhinishwa na vikao vya Dunia Yetu

-Kuandaa na kusambaza taarifa za fedha kwa wanachama kila mwezi kupitia njia za mtandao kama vile barua pepe, WhatsApp, nk.

22. *Mikutano ya Chama*

(1) Uongozi na usimamizi wa shughuli za Chama utafanywa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika na Masharti ya Chama kwa maslahi ya mwanachama ambapo mamlaka ya juu ya Uongozi na Usimamizi wa shughuli zote za Chama yatakuwa mikononi mwa wanachama kupitia Mikutano halali ya Chama.

(2) Vikao vya Dunia Yetu vitafanyika mara nne kwa mwaka, kila baada ya miezi mitatu.

(3)Mkutano Mkuu wa uchaguzi utafanyika kila baada ya miaka mitatu.

(4)Mwanachama ambaye hatahudhuria vikao vitatu mfululizo bila sababu ya msingi (kama kazi, ugonjwa, safari, au msiba) atachukuliwa kama kajiuzulu na atahitaji kuomba upya uanachama baada ya miezi 6. Michango yake haitarudishwa.

(5)Katibu atahitajika kuwasilisha taarifa za mahudhurio katika kila kikao.

(6)Wanachama walioko nje ya Dar es Salaam watapokea taarifa za vikao kwa njia ya mtandao na wanatarajiwa kutoa maoni yao kupitia njia hiyo au kutuma ujumbe kwenye simu.

(7)Wanachama wanatarajiwa kushiriki katika shughuli zote za Dunia Yetu bila kubagua shughuli yoyote.

23. *Mkutano Mkuu wa Chama na Wajumbe*

(1)Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama watakuwa ni wanachama wote katika Chama. Pamoja na majukumu yaliyoainishwa katika Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika Mkutano Mkuu wa Chama utakuwa na majukumu yafuatayo:-

- Kusoma na kuthibitisha mihutasari ya Mikutano Mikuu ya Mwaka iliyopita; na

- Kupokea na kupitia taarifa za fedha za Mwaka pamoja na taarifa za mkaguzi wa nje wa hesabu na taarifa nyingine muhimu kwa maendeleo ya Chama.

24. *Kamati ya Fedha na Usimamizi wa Bajeti*

(1) Mwaka wa fedha wa Chama utaanza tarehe 01 Julai hadi tarehe 30 Juni Mwakani;

(2)Kamati hii maalum itakuwa na majukumu matatu ya msingi:

a.Kupendekeza na kufuatilia uwekezaji

b.Kufanya ukaguzi wa fedha za Dunia Yetu

c.Kutoa makadirio ya mapato na matumizi kila mwaka na kupanga bajeti ya mwaka

25. *Ushughulikiaji wa Malalamiko na Migogoro*

(1) Mgogoro wowote unaohusu shughuli za Chama kati ya mwanachama wake au watu wanaowalalamikia, au kati ya mwanachama au watu ambao wanadaiwa na Bodi au Afisa yeyote, au kati ya Chama na Chama cha Ushirika kingine au Mtoa Huduma utasuluhishwa kwa njia ya amani kupitia majadiliano au maridhiano.

(2) Ikiwa mgogoro chini ya sharti dogo la (1) haujasuluhishwa kwa amani ndani ya siku 30, mgogoro huo utapelekwa kwa Mrajis kwa usuluhishi kupitia Fomu Na. 13 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni za Vyama Vya Ushirika.

(3) Kupelekwa kwa usuluhishi chini ya sharti dogo la (2) kunaweza kufanywa na Bodi au Chama kwa azimio la Mkutano Mkuu au na mhusika yeyote katika mgogoro, au na mwanachama yeyote wa Chama kama mgogoro unamhusu Mjumbe wa Bodi kudaiwa kiasi cha fedha na Chama.

(4) Katika kupeleka mgogoro kwa Mrajis chini ya sharti dogo la 3 mlalamikaji atapaswa kupeleka nakala ya marejeo kwa ajili ya mlalamikiwa.

(5) Katika kupokea marejeo chini ya sharti dogo la (2), Mrajis ataweka tarehe ya kupokea na kutuma nakala kwa mlalamikiwa na wahusika wote ambao kwa maoni yake mgogoro huo unawahusu.

(6) Baada ya kupokea marejeo ya mgogoro katika sharti dogo la (5), mlalamikiwa atapaswa ndani ya siku kumi na tano tokea tarehe ya kupokea, kuwasilisha maelezo ya kujibu kwa Mrajis.

(7) Taratibu nyingine za utatuzi wa migogoro baada ya hatua ya sharti dogo la (6) zitafanyika kwa kuzingatia Kanuni za Vyama Vya Ushirika.

26. *Kuvunjika kwa Chama*

Bila kuathiri sababu za kuvunjika kwa Chama kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika, Chama kinaweza kuvunjika iwapo:2-

a)Chama kitafutwa katika daftari la Vyama Vya Ushirika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika;

b)Vyama mwanachama vitaazimia Chama kuvunjwa kwa Azimio la robo tatu (3/4) ya wajumbe wote katika Mkutano Mkuu;

27. *Kurekebisha Masharti*

Masharti haya yanaweza kufanyiwa marekebisho kwa maamuzi ya robo tatu ya kupitia uongozi wa Bodi na kupelekwa kwa mwanachama katika Mkutano Mkuu na kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika Sheria na Kanuni za Vyama Vya Ushirika

28. *Mengineyo*

Uidhinishaji na uwekaji saini kumbukumbu za Chama: Kumbukumbu zote za kudumu na mikataba ya Chama itasainiwa na Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti kama wote hawapo Meneja na Mjumbe mmoja wa Bodi watatia saini.

29. *Kuidhinishwa na kuanza kutumika kwa Masharti*

Masharti haya hayatakuwa halali na kuanza kutumika kabla ya kupitishwa na kuungwa mkono na Wajumbe wa Mkutano Mkuu Anzilishi na baada ya kuidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis wa Vyama Vya Ushirika.

**MASHARTI HAYA YAMEANDALIWA NA KUPITISHWA KWENYE MKUTANO NA WANACHAMA WAANZILISHI KUMI (10) :**

| | JINA | UMRI | ANUANI YA MAKAZI | MTAA | WILAYA | SAHIHI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Godfrey Mariki | 27 | Mikocheni | Senga Street | Kinondoni | |
| 2 | David Machuche | 28 | Mbezi Juu | Ipasa Close | Kinondoni | |
| 3 | Victor Muhagachi | 27 | Masaki | Mtaa wa Haile Selassie | Kinondoni | |
| 4 | Brian Nderumaki | 28 | Mlalakuwa | Makongo | Kinondoni | |
| 5 | Buyegi Joseph | 27 | Goba | Kwa Olomi | Kinondoni | |
| 6 | Derick Makene | 28 | Changanyikeni | Isaria Street | Kinondoni | |
| 7 | Norman Karamaga | 29 | Victoria Mwananyamala | Noble Center | Kinondoni | |
| 8 | Rose Rwegasira | 25 | Kinondoni | Kimwaga street | Kinondoni | |
| 9 | Kalebu Gwalugano | 24 | Bahari Beach | Dira Street | Kinondoni | |
| 10 | Jumanne Mtambalike | 36 | Victoria Mwananyamala | Noble Center | Kinondoni | |